# HOTUBA YA IJUMAA

## صفات المؤمنين في القرآن الكريم

## Sifa za Waumini ndani ya Quran Tukufu

## Imefasiriwa na

## Profesa Ayman Alasar

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mwenye kusema ndani ya Kitabu cha:

**إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ذَلِكَ الْفَوْزُ الْكَبِيرُ.**

{**Hakika wale walioamini na wakatenda mambo mema basi wana Pepo ipitayo chini yake mito huko ndio kufaulu kukubwa**}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika, na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mja wake na Mtume wake, ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma na amani pamoja na baraka kwake na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale waliowafuata kwa wema mpaka siku ya mwisho.

**Ama baada ya utangulizi huo**:

Hakika Imani ni katika neema kubwa ya Mwenyezi Mungu kwa mwanadamu, ambapo Anasema Mola Mtukufu: **بَلِ اللَّهُ يَمُنُّ عَلَيْكُمْ أَنْ هَدَاكُمْ لِلْإِيمَانِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ**

{**Bali Mwenyezi Mungu ndiye aliye kufanyieni hisani kwa kukuongoeni kwenye Imani, ikiwa nyinyi ni wa kweli**} nayo ndio njia ya kufika kwenye maisha yaliyosalama na matumaini pamoja na mafanikio na malipo makubwa, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُ حَيَاةً طَيِّبَةً وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُم بِأَحْسَنِ مَا كَانُواْ يَعْمَلُونَ.**

{**Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa malipo yao kwa matendo bora waliyo kuwa wakiyatenda**}. Na Akasema tena Mola Mtukufu:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُواْ وَعَمِلُواْ الصَّالِحَاتِ وَأَقَامُواْ الصَّلاَةَ وَآتَوُاْ الزَّكَاةَ لَهُمْ أَجْرُهُمْ عِندَ رَبِّهِمْ وَلاَ خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلاَ هُمْ يَحْزَنُونَ

{**Hakika wale walio amini na wakatenda mema na wakashika Sala na wakatoa Zaka, wao watapata malipo yao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika**}.

Mwenye kuzingatia ndani ya Quran Tukufu anagunduwa kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaelezea Waumini kwa sifa mbalimbali ndani ya kitabu cheka, miongoni mwa sifa hizo ni pamoja na kuendeleza utekelezaji wa Ibada ya swala ndani ya wakati wake, na kutimiza nguzo zake, na unyenyekevu ambapo Anasema Mola Mtukufu:

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ * الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ.

{**Hakika wamefanikiwa Waumini * Ambao ni wanyenyekevu katika Sala zao**}. Na Anasema tena Mola Mtukufu: وَالَّذِينَ هُمْ عَلَى صَلَوَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ {**Na ambao Sala zao wanazihifadhi**}.

Sifa nyengine: Kupuuza mambo ya upuuzi ni sawa sawa yakiwa ni kauli au kitendo ambapo Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: وَالَّذِينَ هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُونَ {**Na wale ambao mambo ya kipuuzi ni wenye kuyapunzia**}, Waumini ni wenye kujitenga na mambo madogo madogo wenye kuyapa uzito makubwa, Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَإِذَا سَمِعُوا اللَّغْوَ أَعْرَضُوا عَنْهُ.

{**Na wanapo sikia upuuzi hujitenga nao**}. Na Anasema tena pia:

وَالَّذِينَ لا يَشْهَدُونَ الزُّورَ وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا.

{**Na wale ambao hawatoi ushahidi wa uwongo, na pindi wapitapo penye upuuzi, hupita kwa heshima yao**}. Na anasema Mtume SAW: مِنْ حُسْنِ إِسْلَامِ المَرْءِ تَرْكُهُ مَا لَا يَعْنِيهِ

“Uislamu mzuri wa mtu ni kuacha yale yasiyo muhusu”.

Mingoni mwa sifa nyengine ni: kutoa, kuamrisha mema, na kukataza maovu, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu: **وَالَّذِينَ هُمْ لِلزَّكَاةِ فَاعِلُونَ** {**Na wale ambao hutekeleza ibada ya zaka**}. Na Anasema tena Mola Mtukufu:

**وَالمُؤمِنونَ وَالمُؤمِناتُ بَعضُهُم أَولِياءُ بَعضٍ يَأمُرونَ بِالمَعروفِ وَيَنهَونَ عَنِ المُنكَرِ وَيُقيمونَ الصَّلاةَ وَيُؤتونَ الزَّكاةَ وَيُطيعونَ اللَّـهَ وَرَسولَهُ أُولـئِكَ سَيَرحَمُهُمُ اللَّـهُ إِنَّ اللَّـهَ عَزيزٌ حَكيمٌ.**

{**Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa waoni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu, na hushika Sala, na hutoa Zaka, na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, Mwenye hekima**}.

Sifa nyengine: Ni kuwa wao ni watu safi na ucha-Mungu ambapo Anasema Mola Mtukufu:

**وَالَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ * إِلَّا عَلَى أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ.**

{**Na ambao wanazilinda tupu zao * Isipokuwa kwa wake zao au kwa iliyo wamiliki mikono yao ya kulia. Kwani hao si wenye kulaumiwa**}. Na Mtume SAW alikuwa akimuomba Mola wake Mtukufu katika maombi yake usafi wa moyo, ambapo alikuwa anasema: **اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الهُدَى وَالتُّقَى والعَفَافَ وَالغِنَى** "Ewe Mwenyezi Mungu hakika yangu ninakuomba uongofu ucha-Mungu usafi wa moyo na kutosheka" na anasema Muhammad Ibn Hanafiah R.A: Ukamilifu ni katika mambo matatu: Usafi wa moyo katika dini, kusubiri juu ya matatizo, na mazingatio mazuri katika maisha.

Sifa nyengine: Kulinda uaminifu, na kutekeleza ahadi, kwani Muumini wa kweli siku zote huahidi uaminifu wake kama vile mkulima anavyoahidi kilimo chake na mfanya kazi uzalishaji wake, kwani Imani na utakelezaji wa ahadi ni vyenye kufungamana ambapo Anasema Mola Mtukufu: **وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمَانَاتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ** {**Na wale ambao uaminifu wao na ahadhi zao wanavichunga**}. Na Anasema Mwenyezi Mungu:

**إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَن تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰأَهْلِهَا.**

{**Hakika Mwenyezi Mungu anawaamrisheni kurudisha amana kwa wenyewe**}, na Mtume wetu SAW ameunganisha kati ya amana na Imani, ambapo anasema:

" لَا إِيمَانَ لِـمَنْ لَا أَمَانَةَ لَهُ، وَلَا دِينَ لِـمَنْ لَا عَهْدَ لَهُ".

"Hana Imani kwa mtu asiye na uaminifu, wala hana dini mtu asiye na ahadi".

**HOTUBA YA PILI**:

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimwendee mbora wa viumbe naye ni Mtume wetu Muhammad SAW pamoja na Watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Miongoni mwa sifa za Waumini: Ni wenye kudumu katika kumtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu na wanafanya vizuri katika kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَى رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ.

{**Hakika Waumini ni wale ambao anapo tajwa MwenyeziMungu nyoyo zao hujaa hofu, na wanapo somewa Aya zake huwazidisha Imani, na wakamtegemea Mola wao Mlezi**}, utegemezi wa kweli ni ukweli wa mja kwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu, wala halikamiliki hilo isipokuwa kwa kuchukuwa sababu za matendo na kufanya juhudi, ambapo anasema Mtume wetu Muhammad SAW:

لَوْ أَنَّكُمْ تَتَوَكَّلُونَ عَلَى اللهِ حَقَّ تَوَكُّلِهِ لَرَزَقَكُمْ كَمَا يَرْزُقُ الطَّيْرَ، تَغْدُو خِمَاصاً وَتَرُوحُ بِطَانًا.

"*Lau nyinyi mungekuwa mnamtegemea kweli Mwenyezi Mungu ukweli wa kumtegemea basi angewaruzuku kama vila anavyowaruzuku ndege, kwani hutoka asubuhi matumbo yao yakiwa hayana kitu na hurudi jioni matumbo yakiwa yamejaa chakula*".

Imani ya kweli athari yeka inaenea kwenye jamii, kwani Muumini wa kweli hawezi kuwa mtu wa kughushi mambo, wala kuwa mtu mnafiki, wala muongo, wala mvunja ahadi na makubaliano wa kuwa mkiukaji, imani ya kweli humjenga mtu kwenye maadili mazuri, Muumni wa kweli ni mkarimu na mpole ambapo Anasema Mwenyezi Mungu:

ثُمَّ كَانَ مِنَ الَّذِينَ آمَنُوا وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا بِالْمَرْحَمَةِ.

{**Tena awe miongoni mwa walio amini na wakausiana kusubiri na wakausiana kuhurumiana**}. Na Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَالْعَصْرِ * إِنَّ الْإِنْسَانَ لَفِي خُسْرٍ * إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ.

{**Naapa kwa Zama * Hakika binadamu bila ya shaka yumo katika khasara * Ila wale walio amini, na wakatenda mema, na wakausiana kwa haki, na wakausiana kusubiri**}. Na anasema Mtume wetu Muhammad SAW:

مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللهِ وَاليَوْمِ الآخِرِ فَلَا يُؤْذِ جَارَهُ، وَمَنْ كَانَ يُؤْمِنُ باللهِ وَاليَوْمِ الآخِرِ فَلْيُكْرِمْ ضَيْفَهُ، وَمَنْ كَانَ يُؤْمِنُ باللهِ وَاليَوْمِ الآخِرِ فَلْيَقُلْ خَيْرًا أَوْ لِيَصْمُتْ.

"*Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na akaamini siku ya mwisho basi asifamfanyie maudhui jirani yake, na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho basi amkirimu mgeni wake, na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho basi na asema mazuri au anyamaze*".

Ni uzuri ulioje tunapojipamba na mafundisho ya Imani, ili itufikia hali ya amani utulivu matumaini na furaha duniani na akhera, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu malipo ya Waumini:

أُولَـئِكَ هُمُ الْوَارِثونَ*الَّذِينَ يَرِثونَ الْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا خَالِدُون.

{**Hao ndio warithi * Ambao watairithi Pepo ya Firdausi, wadumu humo**}. Na Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu:

إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ.

{**Isipokuwa wale walioamini na wakatenda mambo mema hao wana malipo yasiyokwisha**}. Na Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ كَانَتْ لَهُمْ جَنَّاتُ الْفِرْدَوْسِ نُزُلًا * خَالِدِينَ فِيهَا لَا يَبْغُونَ عَنْهَا حِوَلًا.

{**Hakika wale walio amini na wakatenda mema mashukio yao yatakuwa kwenye Pepo za Firdausi * Watadumu humo; hawatataka kuondoka**}.

Ewe Mwenyezi Mungu tupendezeshee Imani na uipambe kwenye nyoyo zetu.

**اللهم آمیین**